

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simuu: 255-262961500/1
Nukushii: 255-262961502
Barua pepe: press@ikulu.go.tz
 Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ikulu, Chamwino.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa masikitiko makubwa ametangaza kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mhe. Benjamin William Mkapa kilichotokea usiku wa kuamkia leo tarehe 24 Julai, 2020.

Mhe. Rais Magufuli amesema Mhe. Benjamin William Mkapa amefariki dunia hospitalini Jijini Dar es Salaam ambako alikuwa akipatiwa matibabu.

Mhe. Rais Magufuli amewataka Watanzania wote kuwa watulivu na wastahimilivu baada ya kupokea taarifa za kuondokewa na mpendwa wao Mhe. Benjamin William Mkapa.

“Kwa masikitiko makubwa tumepata msiba mkubwa, Mzee wetu Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu amefariki dunia, amefariki dunia katika hospitali Jijini Dar es Salaam ambako alikuwa amelazwa, niwaombe Watanzania tulipokee hili, tumepata msiba mkubwa na tuendeleo kumuomba Mzee wetu Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa ambaye ametangulia mbele za haki, taarifa zingine zitaendelea kutolewa lakini Mzee Mkapa hatuanaye tena” amesema Mhe. Rais Magufuli katika taarifa yake kwa Taifa.

Taarifa zingine kuhusiana na msiba huu mkubwa zitatolewa baadaye.

A blue ink signature of Gerson Msigwa, consisting of stylized initials and a long horizontal stroke.

Gerson Msigwa

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, IKULU

Chamwino

24 Julai, 2020